TANGAZO LA SERIKALI NA 34 la Tarehe 24/02/2017

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA, ZA MWAKA 2017

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji wa Mafinga za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelezwa vinginevyo;-

"Ada na Ushuru**"** maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

"Afisa Mwidhiniwa**"** maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Bajaji**"** maana yake pikipiki yenye matairi matatu.

"Bidhaa**"** maana yake ni vitu mbalimbali vinavyoweza kuuzwa na kununuliwa katika duka, soko au eneo la mnada.

"Chombo cha Usafiri**"** maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Mafinga

"Kibali**"** maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

"Kituo cha Mabasi**"** maana yake ni eneo maalum lililotengwa na

Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya Abiria ;

‘‘Kukodi’’ maana yake ni kuazima mali ya Halmashauri kulingana na viwango vya fedha vilivyowekwa.

“Machinjio**”** maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi ya wanyama waliochinjwa ;

“Madini ya ujenzi**”** maana yake ni Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri ambayo hutumika kwa shughuli za ujenzi na itahusisha pia tofari za kuchoma ;

‘‘Magari ya abiria’’ maana yake ni mabasi makubwa na madogo, na magari mengine yote yanayojishughurisha na kubeba abiria kama Noa, na Landrover ;

‘‘Matangazo**’’** maana yake ni maandishi yoyote yaliyoandikwa au kubandikwa kwenye vibao, ukuta wa jengo, nguzo, au chombo chochote kwa ajili ya kutangaza biashara ;

‘‘Mazao**’’** maana yake ni mazao yote ya kilimo na mazao yote ya misitu ;

‘‘Mazao ya misitu’’ maana yake ni magogo, mbao, mirunda, nguzo, fito, mkaa, matawi, vumbi la mbao, asali na zao lolote litokanalo na misitu.

‘‘Mgeni’’ maana yake ni mtu ambaye baada ya kulipa kiasi cha fedha anamilikishwa chumba au vyumba katika nyumba ya kulala wageni kwa muda wa siku nzima au muda mfupi katika siku.

“Mkurugenzi**”** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“Mnada**”** maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa.

‘‘Mnunuzi**’’** maana yake ni mtu binafsi, Shirika, Taasisi, Kampuni, Chama au Ushirika atakayenunua mazao au bidhaa kwa muuzaji, itamuhusisha pia mtu anayesafirisha mazao nje ya Halmashauri.

‘‘Mnyama’’ maana yake ni ng’ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe au mnyama yeyote anayefugwa na binadamu.

‘‘Muuzaji’’ maana yake ni mtu binafsi, Shirika, Taasisi, Kampuni, Chama au Ushirika atakayeuza mazao au bidhaa katika soko

linalomikiwa na Halmashauri.

''Soko'' maana yake ni sehemu maalum (iliyojengwa au isiyojengwa) iliyotengwa na inamilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua mazao au bidhaa yoyote kufuatana na taratibu zilizowekwa na Halmashauri na inajumuisha pamoja na gulio, minada na masoko ya mbao.

"Stendi'' maana yake ni sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda ili kushusha, kupakia abiria na mizigo.

"Wakala" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

SEHEMU YA II
NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa kwa viwango vilivyoonyeshwa kwenye majedwali ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Halmashauri itatenga maeneo maalumu ya kutoza Ada na Ushuru kutokana na chanzo husika.

(4) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

5.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

(3) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri/ Wakala na mlipa Ada na ushuru.

Uteuzi wa Wakala

6. Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua mtu binafsi, kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa Wakala

7.-(1) Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa-

(a) Kukusanya na kupokea Ada na Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya Mkataba wa uwakala;

(c) Wakala aliyeteuliwa kukusanya mapato ya Halmashauri atatakiwa kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla ya kusaini Mkataba.

(d) Kusanyo la mwezi mmoja lililowekwa dhamana na wakala litarejeshwa mwisho wa mwaka wa fedha unahusika na Mkataba.

(e) Kuilipa Halmashauri kiwango cha uwakala kilichokubaliwa katika mkataba siku tano (5) kabla ya tarehe ya kuanza uwakala Kwa kila mwezi;

Ushuru wa stendi ya mabasi

8.-(1) Halmashauri itatoza Ushuru wa stendi utakaokusanywa kutoka kwa kila mmiliki wa gari la abiria linalotoka kituo kimoja au linaloanzia na kupitia kwenye kituo cha mabasi cha Mafinga na vituo vingine vitakavyoanzishwa ndani ya Halmashauri kwa viwango kama vilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Magari yote yanayofanya biashara ya kusafirisha abiria ni lazima yapitie katika kituo cha mabasi kilichoidhinishwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya au kuruhusu mtu mwingine kufanya matengenezo au kujaza mafuta ndani ya kituo cha mabasi.

Ushuru wa Maegesho

9.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa kila gari, bajaji na itakayoegeshwa kwenye sehemu za maegesho kama ilivyo ainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi mitaa yote ya katikati ya mji itakuwa na eneo lake la maegesho na Halmashauri inaweza kugawa maegesho kwa kutumia alama yoyote kuonyesha sehemu ambayo gari linatakiwa kuegeshwa.

(3) Halmashauri itatoza ushuru wa kulaza gari, bajaji au pikipiki kwa kila gari, bajaji au pikipiki itakayoegeshwa usiku kucha kwenye maeneo ya Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(4) Ushuru wa kulaza au maegesho ya magari unaweza kulipwa kwa siku au kwa mwezi na utalipwa mara baada ya gari kuegeshwa, na endapo mtu atakuwa amelipia ushuru wa kulaza au maegesho kwa siku au kwa mwezi ataruhusiwa kuegesha gari lake bila kulipia tena kwa muda aliolipia.

(5) Magari yafuatayo yatasamehewa kulipiwa ushuru wa maegesho chini ya Sheria Ndogo hizi:

(a) magari yote ya wagonjwa (ambulance)
(b) magari ya Serikali na taasisi zake
(c) magari ya Jeshi
(d) magari ya Zimamoto
(e) pikipiki za Serikali.

Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki Halmashauri inaweza kusamehe gari lolote lisilipiwe ushuru wa maegesho endapo Halmashauri itaridhika na sababu alizozitoa mwombaji wa msamaha.

Ushuru wa mbao za matangazo

10.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa mbao za matangazo kwa viwango vilivyotajwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka mbao za matangazo kwenye eneo la Halmashauri bila kibali cha Halmashauri.

Ushuru wa machinjio, ukaguzi wa nyama na kununua ngozi

11.-(1) Kila mnyama atakayechinjwa kwenye machinjio yaliyoidhinishwa na Halmashauri atalipiwa ushuru wa ukaguzi wa nyama na ushuru wa machinjio kwa viwango vilivyoonyeshwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Kila mnunuzi wa ngozi ndani ya Halmashauri atatakiwa kulipa ushuru wa kununua ngozi kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinjia mnyama sehemu ambayo haijaidhinishwa na Halmashauri ikiwa nyama hiyo itakuwa ni kwa matumizi ya watu wengi.

Ushuru wa madini ya ujenzi

12.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa madini ya ujenzi, kutoka kwa wanunuzi wa madini hayo ndani ya mamlaka ya Halmashauri kwa viwango vilivyotajwa katika jedwali la kwanza sehemu "H"ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Mchimbaji yeyote wa Madini ya ujenzi atatakiwa kuzingatia Sheria za Hifadhi ya mazingira, na Halmashauri inaweza kusimamisha shughuli za Uchimbaji iwapo itathibitika kuwa kufanya hivyo ni muhimu ili kudhibiti Uharibifu wa mazingira.

(3) Halmashauri inaweza kuruhusu madini ya ujenzi kuchimbwa na kusombwa bila kulipa ushuru kwa kibali maalum kitakachotolewa na Mkurugenzi.

(4) Madini ya ujenzi yatachimbwa na kusombwa katika maeneo yaliyoidhinishwa na Halmashauri kwa shughuri hiyo.

Ushuru wa mazao

13.-(1) Kutakuwepo na Ushuru wa Mazao ambao utatozwa na kukusanywa na Halmashauri kwa mazao yatakayozalishwa katika eneo la Halmashauri kwa kiwango kisichozidi asilimia tano (5%) ya bei ya kuuzia kwenye chanzo.

(2) Ushuru huo utalipwa na mnunuzi wa mazao kutoka kwenye eneo ambalo zao au mazao hayo yanazalishwa ndani ya Halmashauri.

Ushuru wa masoko na minada

14.-(1) Halmashauri itatoza ushuru kwa bidhaa zinazoingia kwenye masoko ya mazao au bidhaa kwa viwango vilivyotajwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa utumiaji soko kwa viwango kama vilivyotajwa katika Sheria Ndogo hizi.

(3) Halmashauri itatoza ushuru kwa mazao ya misitu yanayoingia kwenye masoko ya mbao kwa viwango vilivyotajwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(4) Halmashauri itatoza ushuru wa bidhaa zinazouzwa minadani kwa viwango vilivyotajwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(5) Halmashauri itatenga maeneo maalum ya minada na masoko kwa ajili ya kuuzia bidhaa husika.

(6) Ni marufuku kwa mtu yeyote kupakua, kupakia au kuuzia bidhaa eneo tofauti na eneo lililotengwa maalum kwa kupakua, kupakia au kuuzia bidhaa hiyo.

Ushuru wa Hoteli

15.-(1) Kila mmiliki wa Nyumba ya kulala wageni anapaswa kulipa asilimia kumi (10%) ya malipo yatolewayo na mgeni kwa huduma aliyoipata kwenye nyumba hiyo ya wageni.

(2) Kila mgeni aliyefika kwa lengo la kupata huduma katika nyumba ya wageni atatakiwa kusajiliwa katika daftari la wageni kila siku au kwa muda huduma ilipotolewa.

Ushuru wa Majengo

16.-(1) Halmashauri baada ya kufanya uthamini wa majengo itatoza ushuru kulingana na thamani ya jengo husika.

(2) Halmashauri itatakiwa kutunza orodha ya majengo yote yaliyofanyiwa uthamini na kila mmiliki au mwakilishi wake anaweza kuomba kuhakiki taarifa za jengo lake.

(3) Bila kuathiri kifungu kidogo (1) hapo juu Halmashauri itatoza ushuru wa majengo yote ambayo hayajafanyiwa uthamini kama ilivyoonyeshwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA III: MENGINEYO

Kukamata mali na kuiuza

17. Mtu yeyote ambaye atakataa kulipa Ada au Ushuru wa mali yake kama ilivyo elekezwa na Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata na kuuza mali hiyo kwa kibali cha Mahakama.

Halmashauri kutowajibika na hasara

18. Halmashauri haitawajibika kwa hasara au uharibifu wowote utakaotokea kwa namna yoyote ile, aidha wakati wa kukusanya madeni au kwa mali zitakazokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama uharibifu huo umetokana na uzembe wa Halmashauri basi Halmashauri itawajibika kwa uharibifu huo

Makosa

19.-(1) Itakuwa ni makosa kwa Wakala yeyote ambaye-

(a) Atakusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;

(b) Atajaribu au atakusanya Ada na Ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo hizi;

(c) Atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

(2) Itakuwa ni makosa kwa Mtu yeyote ambaye-

(a) Atashindwa, atadharau, au atakaidi/ Atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

(c) Atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) Kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) Atajenga jengo lolote ndani ya Halmashauri bila kuwa na kibali cha ujenzi kilichotolewa na mamlaka husika;

(f) atashindwa kuweka Kumbukumbu, Vitabu, Hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; na

(g) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

20. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifisha kosa

21. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) mtu yeyote iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye Jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi na kuwa tayari kulipa ushuru pamoja na faini anayodaiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetungwa chini ya kifungu cha 4 (1))*

SEHEMU "A"

USHURU WA STENDI

	AINA YA GARI	KIWANGO CHA USHURU
1.	Mabasi makubwa	2000/=@siku
2.	Mabasi ya kati	1500/=@siku
3.	Hiace	1000/=@siku
4.	Magari madogo abiria (noah, landrover n.k).	1000/=@siku
5.	Magari madogo mengine	500/=@siku
6.	Gari za mizigo - tani 1-3 - tani 4-10 - tani 10 na kuendelea	 1000/=@siku 2500/=@siku 4000/=@siku
7.	Pikipiki ya magurudumu matatu	500/=@siku
8.	Pikipiki ya magurudumu mawili	500/=@siku

SEHEMU "B"

USHURU WA MAEGESHO

NA	AINA YA GARI	KIWANGO USHURU
1	Gari zaidi ya tani 10	3000/= @siku
2	Gari chini ya tani 10 na zaidi ya tani 1	2000/=@siku
3	Pickup/station wagon	1500/=@siku
4	Gari ndogo	1000/=@siku
5	Bajaji na pikipiki	500/=@siku

Tangazo la Serikali Na. 34 (linaendelea)

SEHEMU "C"

USHURU WA KULAZA GARI MAENEO YANAYOMILIKIWA NA HALMASHAURI

NA	AINA YA GARI	KIWANGO USHURU
1.	Gari zaidi ya tani 10	5000/= @siku
2.	Maroli chini ya tani 10 na zaidi ya tani 1	3500/=@siku
3.	Pickup/station wagon	2000/=@siku
4.	Gari ndogo	1000/=@siku
5.	Pikipiki	1000/=@siku
6.	Mabasi makubwa	3000/=@siku
7.	Mabasi ya kati	2500/=@siku
8.	Mabasi madogo	1500/=@siku
9.	Bajaji na pikipiki za magurudumu matatu	1000/=@siku

SEHEMU "D"

USHURU WA MBAO ZA MATANGAZO

1 Matangazo yanayowaka kwa nguvu za umeme ..... Tshs. 25.000/= kwa mita za mraba @ mwaka.

2 Matangazo ya biashara yasiyowaka kwa nguvu za umeme au yasiyong'aa…….Tshs 20,000/= kwa mita za mraba @ mwaka.

SEHEMU "E"

USHURU WA MACHINJIO

NA	AINA YA MNYAMA	KIWANGO CHA USHURU
1.	Ng'ombe	5500/=@kichwa
2.	Nguruwe	3000/=@kichwa
3.	Mbuzi/Kondoo	1500/=@kichwa

SEHEMU "F"

USHURU YA UKAGUZI WA NYAMA

NA	AINA YA MFUGO	KIWANGO CHA ADA NA USHURU
1.	Ng'ombe	2000/=@kichwa
2.	Nguruwe	1000/=@kichwa
3.	Kondoo/Mbuzi	500/=@kichwa

SEHEMU "G"

USHURU WA KUNUNUA NA KUKUSANYA NGOZI

NA	AINA YA NGOZI	KIWANGO CHA ADA NA USHURU
4.	Ng'ombe	1000/=@ngozi
5.	Kondoo/Mbuzi	500/=@ngozi

Tangazo la Serikali Na. 34 (linaendelea)

SEHEMU "H"

USHURU WA MADINI YA UJENZI

Magari yote yanayobeba madini ya ujenzi yatatakiwa kulipa ushuru wa shilingi 2000/= kwa tripu au 100,000/= kwa mwaka.

SEHEMU "I"

13. USHURU WA BIDHAA ZA SOKONI

NA	ADA YA USHURU	KIWANGO CHA NA USHURU
1.	Mahindi	1000/=@gunia la kilo 90
2.	Maharage	1000/=@gunia la kilo 90
3.	Mpunga	1000/=@ gunia la kilo 75
4.	Dagaa	1000/=@ gunia la kilo 70
6.	Samaki	1000/= @tenga kilo 50
10.	Vitunguu	1000/=@gunia la kilo 70
11.	Alizeti	500/=@ gunia la kilo 40
12.	Kabeji, Machungwa, Miwa, Nanasi,Ndizi,Parachichi	5000/= kwa tani moja
13.	Viazi	1000/=@gunia la kilo 100
14.	Hoho	500/= kwa tenga kilo 50
15.	Karanga	2000/= @gunia la kilo 90
16.	Njegere maganda	1000/=@gunia la kilo 90
17.	Nyanya	1000/=@tenga la kilo 50
18.	Mchele	1000/= @ gunia la kilo 100
19.	Unga	500/=@ gunia la kilo 80

SEHEMU "J"

USHURU WA UTUMIAJI WA SOKO

	AINA YA USHURU	KIWANGO CHA USHURU
1..	Ushuru wa meza	300/=kwa siku

SEHEMU "K"

USHURU WA SOKO LA MBAO

NA	AINA YA ZAO LA MISITU	KIWANGO CHA USHURU
1.	Mbao	100/= kwa ubao mmoja
2.	Mirunda	50/= kwa mrunda
3.	Nguzo za simu	2000/= kwa nguzo
4.	Nguzo za umeme	5000/= kwa nguzo
5.	Kuni	3000/=kwa tani
6.	Mkaa	1000/= kwa gunia la kilo 50
7.	Mabanzi	5000/= kwa tani moja
8.	Mazao mengine ya misitu	5000/= kwa tani moja

SEHEMU "L"

USHURU WA MINADA NA MAGULIO

NA	AINA YA BIDHAA	KIWANGO CHA USHURU
1.	Ng'ombe	5,000/=@ngombe
2.	Kondoo	1,000/=@kondoo
3.	Mbuzi	1,000/=@mbuzi
4.	Bidhaa zinazotengenezwa viwandani/ karakana	500/=@siku
5.	Wauza mitumba	500/=@siku
6.	Wauza bia na vinywaji baridi	1,000/=@siku
7.	Wauza nafaka	500/=@ gunia
8.	Ndege (kuku,bata)	500/=@siku
9.	Pombe za asili	500/=@siku
8.	Wauza madawa ya asili	500/=@siku
9.	Wauza vipuri vya baiskeli,pikipiki,magari	500/=@siku
10.	Wauza dagaa	500/=@siku
11.	Wauza samaki	500/=@siku
12.	Wauza chumvi,nyama na mboga za majani	500/=@siku
13.	Wauza vyungu	500/=@siku
14.	Wauza vyombo vya nyumbani	500/=@siku
15.	Wauza viatu	500/=@siku
16.	Wauza nguo mpya	500/=@siku
17.	Mafundi baiskeli	500/=@siku
18.	Bidhaa nyingine ambazo hazijatajwa	500/=@siku
19.	Mifugo mingine ambayo haijatajwa	500/=@siku
20.	Ng'ombe waliopelekwa na kuingizwa mnadani lakini hawajauzwa	1000/=@Ng'ombe

SEHEMU "M"

USHURU WA MAJENGO

	AINA YA JENGO	MAELEZO KUHUSU HALI YA JENGO	KIWANGO CHA USHURU @ MWAKA
1.	Makazi (lisilo la Ghorofa)	(a) Tofari za kuchomwa au block zilizotengenezwa kwa mchanga na simenti, kuta zimesakafiwa. (b) Tofari za kuchomwa au block zilizotengenezwa kwa mchanga na simenti, kuta hazijasakafiwa kwa nje	20,000/= 15,000/=

		(c) Tofari za tope au kuta za tope na haijasakafikiwa pande zote ndani na nje, imeezekwa kwa bati.	8,000/=
2.	Makazi(lenye ghorofa)	Katikati ya mji na nje ya mji	150,000/=
3.	Biashara na makazi kwa pamoja (lisilo la ghorofa)	(a) Katikati ya mji (b) Nje mji kama kata ya Isalavanu, Bumilayinga na Rungemba	150,000/= 40,000/=
4.	Biashara na makazi kwa pamoja (lenye ghorofa)	Katikati ya mji na nje ya mji	300,000/=
5.	Biashara mchanganyiko (Katikati ya mji na nje ya mji).	Maduka, nyumba za kulala wageni n.k	200,000/=
6.	Biashara - nje ya mji	Mashine za kusaga, nyumba za kulala wageni, maduka na nyumba za kupangisha.	100,000/=
7.	Biashara mchanganyiko lenye ghorofa	Katikati ya mji na nje ya mji	700,000/=
8.	Biashara mchanganyiko	Eneo la maduka (shopping centre)	400,000/=
9.	Kiwanda cha huduma (service industry)	Karakana ndogo, na vilabu vya pombe za kinyeji.	50,000/=
10.	Viwanda vidogo	Kama mashine za kusaga	80,000/=
11.	Kiwanda kikubwa		1,500,000/=
12.	Hoteli	(a) Daraja la juu (high class) (b) Daraja la kawaida (normal class)	400,000/= 200,000/=
13.	Benki		750,000/=
14.	Kituo cha mafuta		150,000/=
15.	Kumbi za sinema		150,000/=
16.	Taasisi	(a) Kubwa (b) Ndogo	750,000/= 250,000/=
17.	Minara ya simu		150,000/=

SEHEMU “N”

ADA YA VIBALI VYA UJENZI

AINA YA UJENZI	KIWANGO CHA ADA NA USHURU (TSHS)
VIWANJA VYOTE VYA MAKAZI	50,000/=.
Taasisi mbalimbali (Shule,Vyuo, Nyumba za ibada,Ofisi mbalimbali, Kumbi)ambazo sio ghorofa	150,000/=

Viwanda vikubwa	500,000/=
Viwanda vidogo	200,000/=
Vituo vya mafuta	500,000/=
Ukarabati	50,000/=
Uzio/fensi	100,000/=
Hifadhi ndogo,Uwanja wa michezo, Hoteli za utalii ambazo sio ghorofa	200,000/=
Nyumba za kulala wageni	150,000/=
Ghorofa -ghorofa 1-3	300,000/=
-ghorofa 4-5	400,000/=
-ghorofa 6 na kuendelea	500,000/=

SEHEMU "O"

ADA YA KUPITISHA MICHORO YA MIPANGO MIJI

AINA YA MCHORO	KIWANGO
Mchoro mpya	300,000/=
Kufanya marekebisho ya mchoro au kubadilisha matumizi	200,000/=

SEHEMU "P"

ADA YA UCHANGIAJI WA HUDUMA ZA USAFI

NA	TAASISI	KIWANGO CHA ADA KWA MWAKA	KIWANGO CHA ADA NA USHURU KWA MWEZI
1.	Taasisi zote na mashirika	300,000/=	30,000/=
2.	Hospitali – binafsi	360,000/=	40,000/=
3.	Viwanda vikubwa	600,000/=	60,000/=
4.	Viwanda vya kuoka mikate[bakery]	300,000/=	30,000/=
5.	Hoteli za kitalii	300,000/=	30,000/=
6.	Migahawa	60,000/=	6,000/=
7.	Useremala	30,000/=	4,000/=
8.	Wauza mbao	50,000/=	6,000/=
9.	Mashine ndogo za kusaga na kukoboa	30,000/=	3,000/=
10.	Duka la jumla	50,000/=	5,000/=
11.	Duka la rejareja	30,000/=	3,,000/=
12.	Ghala/godown.	150,000/=	30,000/=
13.	Viwanda vidogo vya kukamua mafuta	50,000/=	5,000/=

14.	Bucha za samaki/nyama	30,000/=	3,000/=
15.	Machinjio.	300,000/=	30,000/=
16.	Baa na mgahawa.	60,000/=	6,000/=
17.	Mini super market.	120,000/=	15,000/=
18.	Vilabu vya pombe za kienyeji kwa chumba kimoja.	25,000	3,000/=
19.	Nyumba za kuishi.	10,000/=	1,000/=
20.	saluni za me na ke	25,000/=	2,500/=
21.	grocery[mini bar]	25,000/=	2,500/=
22.	nyumba za kulala wageni	60,000/=	6,000/=
23.	vituo vya afya na zahanati	100,000/=	10,000/=
24.	vituo vya mafuta	50,000/=	5,000/=
25.	maduka ya vifaa vya ujenzi na	50,000/=	5,000/=
26.	maduka ya nguo na viatu	60,000/=	5,000/=
27.	maduka ya dawa [pharmacy]	50,000/=	5,000/=
28.	maduka ya dawa muhimu	20,000/=	2,000/=
29.	maduka ya mikate na vitafunwa	10,000	1,000/=
30.	maduka ya vyombo	20,000/=	2,000/=
31.	maduka ya kuuza magodoro na samani	50,000/=	5,000/=

SEHEMU "Q"

ADA YA WATOA HUDUMA KWENYE DHIFA NA SHEREHE MBALIMBALI

NA	AINA YA HUDUMA	KIWANGO CHA ADA**(TSHS)**
1.	Washereheshaji (MC)	10,000/= kwa tukio
2.	Mpiga picha (mnato)	10,000/=kwa tukio
3.	Mpiga za kutembea (video)	10,000/= kwa tukio
4.	Wapambaji wa kumbi za burudani	20,000/= kwa tukio
5.	Muziki (DJ)	10,000/= kwa tukio
6.	Mtoa huduma ya Chakula	20,000/=kwa tukio
7.	Wamiliki wa Kumbi za starehe	50,000/= kwa tukio
8.	Upigaji wa disco	30,000= kwa tukio
9.	Disco- live band kutoka nje ya Halmashauri	50,000= kwa tukio
10.	Matangazo ya barabarani ya biashara yanayotumia vyombo vya muziki	20,000/= kwa tukio

———

Tangazo la Serikali Na. 34 (linaendelea)

JEDWALI LA PILI

———

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 21)

Mimi ……wa S.L.P…….ninayefanya biashara katika eneo la……..lilolopo ndani ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga. Nakiri kuwa leo tarehe……..nilikiuka kifungu cha …….cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji wa Mafinga za mwaka 2017. Kwa hiyo kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa wala kushurutishwa na mtu yeyote, nakubali kulipa kiasi cha ushuru ninodaiwa pamoja na faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 22 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini: ……

Mbele yangu……..(Jina)

Saini……

Wadhifa…….

Muhuri wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 29 Aprili 2016 na ilibandikwa mbele ya:

SAADA S, MWARUKA,
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji wa Mafinga

CHARLES JOHN MAKOGA,
Mwenyekiti
Halmashauri ya Mji wa Mafinga

NAKUBALI,

Dodoma,
9 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.)
Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI